IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Jackline N. Murimi,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*


# UTAMAUSHI WA WANAFUNZI SHULENI KATIKA RIWAYA ZA KISWAHILI: *KIDAGAA KIMEMWOZEA* NA CHOZI LA HERI

***Jackline N. Murimi, Chuo Kikuu cha Tom Mboya na***

***Edith Muthoni Mwangi, Chuo Kikuu cha Mount Kenya***

## IKISIRI

Mnamo karne moja iliyopita,elimu ilitolewa na wazee waliokomaa kwenye mazingira yasiyokuwa rasmi mathalani chini ya miti. Wanafunzi na 'walimu' hawa walilazimika kuketi pamoja kulingana na jinsia yao. Hata hivyo, jinsi siku zilivyosonga ndivyo masuala ya elimu yalivyobadilika na ambapo elimu ilifanywa kuwa rasmi. Walimu walipaswa kupitishwa kwenye kozi ya ufundishaji, muda maalum wa kufundishwa ulitengwa na mahali maalum kujengwa kwa ajili ya wanafunzi hawa kukusanyika wakati uliotengwa. Mahali kulikojengwa baadaye kulipewa jina mpya la 'shule'. Jinsi miaka ilivyosonga ndivyo elimu shuleni ilivyoanza kutiliwa maanani na kulazimu watoto kujiunga nayo kwa wingi. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa mwishoni mwa karne ya ishirini na mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja baadhi ya wanafunzi wanazidi kutamaushwa na elimu na hivyo kuiambaa. Je, tatizo liko wapi ?

Utafiti huu ulikusudia kuchanganua sababu za wanafunzi kutamaushwa na elimu shuleni kwa mujibu wa riwaya za *KidagaaKimemwozea* ya Ken Walibora na *ChozilaHeri* ya Assumpta Matei. Kwa minajili ya kuafikia kusudio la utafiti wake, utafiti uliongozwa na malengo mahususi ambayo ni ; kujadili sababu zinazochochea wanafunzi watamaushwe na elimu shuleni kwa mujibu wa riwaya teule na kisha kuchanganua njia mbadala zinazopendekezwa na waandishi kupunguza utamaushi wa elimu kwa wanafunzi shuleni kwa mujibu wa riwaya hizi teule.

Ili kupata data ya utafiti huu, mtafiti alitalii maktaba ili kusoma kazi za fasihi za waandishi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu mada ya elimu kwa jumla. Mtafiti alikuwa na lengo la kusaka vitabu, magazeti, majarida pamoja na tasnifu za watafiti mbalimbali. Vile vile, mtafiti alisakura mitandaoni ili kuboresha data yake kwa kuangazia kazi za wasomi tofauti duniani kuhusu suala hili muhimu la elimu na faida zake kwa jamii ya mwanadamu.

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia na ambapo sifa zake zilitumika kushughulikia masuala halisi ya utamaushi wa elimu kwa wanafunzi shuleni jinsi inavyoshuhudiwa katika jamii ya leo kama ilivyoangaziwa kwenye vitabu teule. Ukusanyaji wa data ulipofikia hatima yake, mbinu ya kimaelezo ilitumika ili kuchambua data jinsi ilivyo na kisha ikawasilishwa kwa lugha ya nadhari huku mtafiti akizingatia malengo aliyokusudia. Kuna Imani isiyoterereka kuwa baada ya utafiti huu kufikia hatima yake, data iliyozalishwa itarutubisha maarifa yaliyoasisiwa na waandishi waliotangulia kuhusu masuala ya elimu na jinsi wanafunzi wa karne ya leo wanavyozidi kuchoshwa na elimu na kukata tamaa siku baada ya siku.

**Utangulizi**

Kulingana Nanestory J (2019), elimu ni tendo au uzoefu wenye athari ya kujenga akili, tabia au uwezo wa kimaumbile wa mtu binafsi. Elimu ni njia ya kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kizazi hadi kingine. Kulingana na historia ya ulimwengu, elimu kama ulivyo utamadani wa mwanadamu, ilianza karne nyingi zilizopita kabla ya Masihi. Pindi tu binadamu alipoanza kuwepo duniani, nayo elimu ilianza kwani ingemsaidia kupitisha ujuzi na maarifa kutoka kizazi hadi kizazi. Ilibidi wakubwa wapitishe ujuzi na maarifa waliyokuwa nayo kwa wadogo wao ili kukidhi mahitaji ya kimsingi. Kubadilika kwa utamadani wa binadamu kulijikita katika uzoefu wa elimu ilivyopitishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Jinsi lugha ya mazungumzo ilivyozidi kupanuka, ndivyo ishara na herufi zilivyoanza kuwa stadi kwa minajili ya kukidhi upana wa elimu. Ishara na herufi hizi zilihitajika kuhifadhi na kupitisha elimu na maarifa siku baada ya siku. Kubadilika na kukua kwa ubongo wa binadamu, kulichochea upanuzi wa elimu ya ujuzi kwenye nyanja tofauti zikiwemo biashara, mawasiliano, ukusanyaji wa chakula, tunu za jamii pamoja na desturi za kidini zilizojenga Imani kuelekea Muumba na hali tata ya kimaumbile. Upekuzi wa kina wa wanahistoria, unadhihirisha kuwa muundo wa elimu na masomo zilikuwa zimeanza nchini Misri kati ya 3000 na 500KK.

Elimu na masomo haya zilizidi kusabazwa ulimwenguni na ikawa katikati ya karne ya kumi, Mabara ya Asia, Ulaya na Marekani yalikuwa yameanza kukubatia mtindo mpya wa elimu rasmi. Ingawa elimu na masomo rasmi zilianza kupokezwa kwa kushtukia tu, baada ya zama za giza ziliboreshwa na kuwa na madarasa na muda fulani uliotengwa kwa kuzipisha. Kabla ya vita vya kwanza vya dunia (1914), wanasayansi walikuwa wametumia elimu ya ujuzi na maarifa kuvumbua teknolojia mpya kwenye nyanja za mawasiliano, usafiri na viwanda. Teknolojia hii ndiyo iliyotumika kuunda zana za vita zilizotumika wakati wa vita vya dunia. Baada ya vita vya pili vya dunia (1945), Shirika la Umoja wa Kimataifa (UN) liliunda na kuibuka na elimu rasmi kama mojawake ya nguzo yake kuu. Kila mtoto ana haki ya kupata elimu.

**Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Wambui, H (2017) huku akiangazia uhusiano wa mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi wa shule za msingi za umma kwenye kaunti ndogo ya Kisumu Mashariki, anaeleza kuwa walimu wengi hutumia njia za mhadhara katika kufundisha kwao kwa sarufi huku mbinu za kisasa zinazowashirikisha wanafunzi zikipuuzwa. Pia, Wambui anaeleza kuwa matumizi ya chaki na ubao yalitawala utaratibu wa kufundisha huku vifaa vingi vikikosa kutumika. Hali hii inawafanya wanafunzi wengi kukosa kuelewa kinachofunzwa kwani asilimia pana ya wanafunzi huelewa kwa kutazama vifaa halisi bali sio kwa kuelezwa kwa kinywa. Hali hii ya kutoelewa inawafanya baadhi ya wanafunzi kukata tamaa na kutamaushwa na elimu shuleni kwani hawaoni faida yake. Kazi hii ya Wambui ilijenga msingi dhabiti kwa kazi ya mtafiti kwani inaangazia chanzo kimoja kinachowafanya wanafunzi na haswa wa shule za msingi wakate tamaa na kutoroka shule. Tofauti ya kazi hii na aliyokusudia kutekeleza mtafiti ni kuwa mtafiti alijikita kwenye riwaya teule kuangazia viwango vyote vya elimu bali sio shule za msingi pekee huku akiangazia sababu za wanafunzi kutamaushwa na elimu, athari zake na mbinu mwafaka za kukabiliana na hali hii kwenye viwango hivi.

Mohochi, E, Mukuthuria, M na Omari, J (2019) huku wakiangazia ufundishaji wa kiswahili katika kambi za Kakuma na Dadaab, wanatambua kuwa wanafunzi wamegawanywa na

kuishi kwa kambi ndogo ndogo kulingana na mataifa walimotoka kwa sababu ya utofauti wa utamaduni wao. Wasomi hawa walitambua kuwa wanafunzi hawa hukubana na changamoto chungu nzima zikiwemo uhaba wa walimu wa kutosha, barabara mbovu, mazingira chafu na ukosefu wa usalama jambo ambalo linakatisha wanafunzi tamaa na wengine wao kutafuta mbinu za kutoroka na kupotelea miji iliyoko karibu kama vile Lodwar, Lokichar, Balabala na Garissa mtawalia. Utafiti wa wasomi hawa ulikuwa na nguzo bora kwa kazi ya mtafiti kwani wanaguzia changamoto zinazowafanya wanafunzi kukata tamaa na kutoroka shule. Licha ya kuwa na msingi huu bora, utafiti huu ni wa nyanjani kinyume na utafiti alioufanya mtafiti ambao ni wa vitabu teule ili kuzamia sababu za utoro huu, athari zake kwa jamii pamoja na mbinu mwafaka za kukabiliana na hali hii nyeti.

Mirianga, R (2014), katika utafiti wake kuhusu mielekeo ya walimu wa shule za msingi kuhusu suala la lugha kama linavyoelekezwa katika katiba ya kenya, anaeleza kuwa wanafunzi wengi hulazimishwa kusoma na kuelewa lugha za kigeni kinyume na matakwa yao na hivyo basi kuwa na mielekeo hasi kuhusu lugha hizo na masomo kwa jumla. Msomi huyu anaeleza kuwa kwa vile wanafunzi wengi hawana uso wa kukabilana na walimu wao moja kwa moja na kueleza hali yao, wanaamua kuruka vizingiti vya shule na kupotelea kusikojulikana. Hali hii inafififisha matumaini ya wazazi kwani wanafunzi hawa ndio tegemeo lao la kesho. Kazi ya Mirianga ilifaa mtafiti kwani inaeleza kiini muhimu sana cha utamaushi wa elimu shuleni, yaani wanapolazimishwa kuelewa wasichokifahamu haswa shule za msingi. Tofauti na kazi yetu ni kuwa mtafiti alijikita kwenye riwaya teule kuangazia viwango vyote vya elimu kutoka shule za msingi hadi vyuo vikuu ili kubaini kwa nini wanafunzi wanakatishwa tamaa na elimu ya shuleni, athari za hali hii kwa jamii zao pamoja na mbinu anuwai za kukabiliana na hali hii.

Barasa, R (2018) katika tasnifu yake kuhusu mielekeo ya wanafunzi na wadau wengine wa shule za sekondari kuhusu sheng: kifani cha shule ya upili ya Jamhuri, Nairobi, anaeleza kuwa matumizi ya lugha ya sheng' yamekuwa changamoto kwa wanafunzi wengi kwani huishia kupata matokeo duni kwenye mitihani yao. Hii ni kwa sababu sheng' haijaruhusiwa kujibu maswali kwenye mitihani na hivyo basi wanapoitumia wanafeli moja kwa moja jambo ambalo linawakatisha tamaa ya kuzidi na masomo shuleni. Kufeli kwao kunawafanya watamaushwe na masomo na hivyo kuamua kutoroka hata kabla ya kukamilisha kiwango cha shule ya upili. Baadaye inakuwa vigumu kurudi shule na hivyo basi hutokomea tu kwenye lindi la masaibu ya kila aina. Kazi ya Barasa ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa kazi ya mtafiti kwani inadokeza sababu moja muhimu ya wanafunzi kutamaushwa na elimu shuleni na haswa shule za upili. Tofauti na kazi aliyonuia kutekeleza mtafiti ni kuwa yeye aliepuka kutembelea shule yoyote ya upili na kujikita kwenye riwaya teule ili kug'amua ukweli wa ongezeko la utamaushi wa elimu shuleni miongoni mwa wanafunzi, athari zake na njia mwafaka za kupunguza ongezeko hili.

Matowo,R (2022) mwandishi wa Habari wa Kituo cha Mwananchi Nchini Tanzania, ameripoti kuwa baadhi ya sababu zinazochangia utamaushi wa wanafunzi shuleni ni uchimbaji mdogo wa dhahabu, kilimo, uvuvi, uzembe wa walimu na kutowajibika kwa wazazi na jamii kwa jumla. Hali hii imechangia nusu ya wanafunzi kukosekana shuleni kwa siku moja. Mwanahabari huyu anapendekeza kuwa mabadiliko murua yanahitajika kwenye sekta ya elimu ili kukabili uzito wa hali hii. Mtafiti anaona umuhimu wa kazi hii kwa kazi yake kwani inadokeza visababishi vya kukata tamaa ya masomo shuleni kwa wanafunzi katika nchi jirani. Huu ni utafiti wa nyanjani ila utafiti aliokusudia kutekeleza mtafiti ni wa riwaya teule ili kubabua sababu za wengi wa wanafunzi kukosekana shuleni, athari zake kwa jamii za wanafunzi hawa pamoja na mbinu zifaazo za kupambana na hali hii.

Ogola,O. (1990) katika utafiti wake uliochunguza sababu za wanafunzi wengi kutoroka shule za upili za umma jijini Nairobi,alieleza kuwa wanafunzi hawa hukubana na uhasama kati yao na walimu ambao huwaadhibu kwa viboko na kazi ngumu shuleni. Kupitia kwa wanafunzi watoro waliohojiwa,Ogola anaeleza kuwa wanafunzi hawa huonewa na walimu wao hali inayosababisha wao kuwa na wakati mgumu pale shuleni hivyo basi wao huishia kufanya maamuzi ya kutoroka shuleni na pia nyumbani mwao na kuishia mitaani. Kazi ya Ogola ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa utafiti huu kwani ilieleza baadhi ya sababu zinazofanya wanafunzi kukatizwa tamaa na elimu ya shuleni na hivyo kuikimbia. Kile ambacho hakufafanua ogola ni athari za utamaushi na utoro wa wanafunzi hawa shuleni pamoja na njia za kukabiliana na suala hili tata. Haya ndiyo mapengo yaliyokusudiwa na utafiti huu kwa kuzingatia riwaya mbili teule. Pia kazi ya Ogola ilijikita nyanjani ilhali utafiti huu ulikuwa wa maktabaani kuliko na matini na vitabu vinavyojadili changamoto zinazokumba mazingira ya elimu shuleni.

Kulingana na kazi ambazo mtafiti ameangazia hapo juu, inabainika kuwa ingawa kuna tafiti nyingi zilizoshughulika na suala la elimu ya shuleni miongoni mwa wanafunzi katika jamii, bado kuna pengo linolihitajika kujazwa kwani kila kazi imeshughulikia suala la elimu kwa jumla tu bila kuangazia sababu zinazochochea wanafunzi wengi kutamaushwa na elimu shuleni, athari zake kwa jamii athiriwa pamoja na njia za kukabiliana na hali hii inayotishia kulemaza elimu kwenye jamii ya leo. Vile vile, hata kama waandishi tofauti wameangazia elimu na masomo kwa jumla, wameshughulikia kipengele kimoja kimoja tu labda kiini, athari au njia za kukabiliana na changamoto za elimu kwenye viwango tofauti tofauti. Hivyo basi, mtafiti alinuia kuangazia vipengele vyote vitatu vinavyohusiana na ukataji tamaa huu huku akiangazia yanayochosha wanafunzi shuleni kiasi cha kufikia maamuzi ya kukata tamaa na kuacha masomo, athari za uchovu huu wa elimu shuleni kwa jamii athiriwa pamoja na njia za kukabiliana na hali hii huku akijikita kwenye riwaya mbili teule ; ile ya Ken Walibora *Kidagaa Kimemwozea*na *Chozi La Heri.*

## SABABU ZA WANAFUNZI KUTAMAUSHWA NA ELIMU YA SHULENI

### Ukosefu wa Karo Kutokana na Umasikini.

Karo ni malipo anayotoa mwanafunzi katika shule ili kugharamia elimu yake. Kulingana na sheria zozote za elimu shuleni,ni lazima kila mwanafunzi kutoa malipo haya ili apate nafasi ya kuendeleza elimu yake la sivyo elimu yenyewe itakatikia katikati. Katika jamii nyingi,karo hulipwa kwa kutumia fedha au mali yoyote asilia kulingana na makubalianoyaliyowekwa.Ukosefu wa karo unaweza kutokana na kupungukiwa na rasilimali au umasikini. Endapo kutakuwa na kutolipwa kwa malipo haya basi kuna uwezekano mkubwa wa elimu ya shuleni kufikia kikomo kwa mwanafunzi na kumfanya atoroke kwa hiari yake au kwa uchungu. Miaka ya hivi karibuni,ukosefu wa karo miongoni mwa wanafunzi umeonekana kuwatamausha wanafunzi wengi jambo linalowafanya kukatiza elimu yao ya shuleni bila kutarajia. Kulingana na ripoti iliyotolewa na Wizara ya Elimu nchini Kenya mnamo Januari 2023 ilibainika kwamba wanafunzi zaidi ya laki mbili hukosa kujiunga na kidato cha kwanza kila mwaka kwa sababu ya ukosefu wa karo. Hali hii hubidi wazazi wa watoto hawa kutafuta ufadhili wa makampuni,mashirika ya humu nchini na yale ya kimataifa na hata kutoka kwa watu binafsi. Uvumbuzi wa ripoti hii unakwenda sambamba tu na yaliyobainika katika utafiti uliofanywa na mtafiti katika riwaya mbili teule.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *KidagaaKimemwozea*anamwangazia Imani na ndugu yake Oscar Kambona ambao walitamaushwa na masomo ya shuleni baada ya mama yao kukosa fedha na hivyo kushindwa kuwalipia karo. Hali hii iliwalazimu Imani na ndugu yake kuishi nyumbani na mama yao hadi pale walipovamiwa na askari waliokuwa wametumwa na 'mwenye shamba' kuwafukuza kutoka kwashamba lao. Hii ni licha ya kuwa imani alikuwa na ndoto kuu ya kusoma hadi chuokikuu na kuwa daktari wa kuwatibu wagonjwa.Haya yanadhihirika kupitia kwa maneno ya imani kwa rafiki yake amani kwenye dondoo hii;

> *"Mama alikuwa na uchefuchefu wa fedha akashindwa kutulipia karo hali ambayo ilinifanya nisononeke sana masomo yangu yalipokatizwa nilipokuwa kwenye mpaka kati ya shule ya msingi na ile ya upili"(KK-uk56)*

Kwingineko, Assumpta Matei katika riwaya yake ya *ChozilaHeri* anamwangazia mwanafunzi wa kike Kairu ambaye hali ya umasikini wa mama yake unaonekana kunyong'onyeza matumaini yake ya kuandama elimu. Kairu anawajulisha wenzake kuwa inabidi mama yake masikini afanye biashara duni ya kuuza samaki kwenye mazingira duni ili kupata karo ya kuelimisha watoto wake. Ukosefu wa matumaini ya kairu kuelimika inajitokeza katika dondoo ifuatayo;

> *''Kwa masikini kama mama ambaye hana mtaji wa kuanzisha biashara ya maana maisha yamekuwa magumu kwetu. Imebidi mama kumlilia mwalimu mkuu ili amruhusu alipe karo kidogokidogo hadi mwisho wa mwaka'' (CLH- uk 93)*

Uchunguzi katika vitabu teule umebaini kuwa ukosefu wa karo unachangia pakubwa ongezeko la wanafunzi wengi kutamaushwa na elimu ya shule na hivyo basi kuiambaa

**Dhuluma Kutoka kwa Wazazi na Walezi**

Dhuluma ni hali ya kutokipa kiumbe haki yake au kukitesa kimwili au kisaikolojia. Kiumbe kinapodhulumiwa, huenda kikafikia maamuzi mazito yasiyotarajiwa na kukifanya kikatishwe tamaa na jambo fulani. Dhuluma miongoni mwa binadamu sio jambo geni katika jamii hali ambayo kwa mara nyingi humfanya binadamu huyu kutamaushwa na mazingira anamoishi na kufikia makataa ya kufanya maamuzi mazito maishani yakiwemo ya kutoroka anamoishi na kufuata mkondo wake wa maisha. Wakati mwingine watoto hudhulumikia mikononi mwa wazazi au walezi wao pale ambapo wazazi hao wanapokosana wao kwa wao na hivyo kutelekeza watoto wanaowategemea. Vijana wengi na haswa wanafunzi huonekana kuathirika sana na dhuluma wanazopitishwa na wazazi na walezi wao jambo ambalo mara nyingi huwalazimu kukatisha elimu yao ya shuleni. Kutokana na ripoti iliyookotwa na kuripotiwa na Shirika la Utangazaji la runinga ya Citizen katika kaunti ya Makueni mnamo mwezi wa Machi mwaka huu, ilibainika kuwa dhuluma za kijinsia zinazopitiwa na baadhi ya watoto hubidi kukatizwa tamaa na masomo ya shuleni na kuacha shule katika kaunti hii kutokana na kutelekezwa na wazazi wanaozozana kuhusu atakayelipa karo na ambao mara nyingi wazazi wao wanaohitilafiana huishia katika kiwango cha kutengana. Hali hii huzima ndoto nyingi za wanafunzi ambao mara nyingi hulazimika kufanya vibarua ili kupata karo za kugharamia masomo yao. Bidii zao huwalazimisha kufanya kazi bila kulipwa chochote ili baada ya muda fulani alichofanyia kazi kitumike kulipia karo zao shuleni. Ripoti ya shirika la Citizen inakwenda sambamba na utafiti uliofanywa na mtafiti kutoka kwa vitabu viwili vya fasihi.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Jackline N. Murimi, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Assumpta Matei katika riwaya yake ya Chozi la Heri anamwangazia Sauna ambaye alidhulumiwa kimapenzi na baba yake wa kambo kisa ambacho kilimlazimu kukatiza masomo yake kwa ghafla. Hii ni kwa sababu dhuluma za kimapenzi kutoka kwa baba yake Maya zilimfanya kuwa mjamzito lakini kitoto kikatunguliwa hata kabla ya kuumbika. Hali hii ilisagasaga heshima ya Sauna kwa wazazi wake kwani alihisi kahujumika kimapenzi na kihisia na hivyo kukosa hamu ya kuendelea na masomo yake. Hili dai linadhihirika kwenye kauli ya maneno ya Sauna kama ifuatayo;

> *‘‘Nilitaka kutokomea kokote kule kwani sikuwa na cha kujivunia. Heshima yangu kwa kwa wazazi walikuwa wameisagasaga na kufanya usuli niliojivunia kuwa bandia. Sikuwa na matumaini wala hamu ya kuendelea na masomo yangu kwani vitendo hivyo vilinihujumu kimapenzi na kihisia’’ (CLH-uk 156)*

Vile vile, Matei anamwangazia Pete msichana wa shule ambaye alilazimika kukatiza elimu yake ya shuleni akiwa darasa lasaba. Kisa na maana, alidhuliwa na mama yake pamoja na wajomba wake waliopokea posa na mahari kutoka kwa mzee Fungo na kumwoza kama mke wa nne. Licha ya Pete kutetewa na nyanya yake kwa kudai kuwa alikuwa na hamu ya kufuatilia elimu, maneno ya bibi huyu yaliangukia masikio yaliyotiwa uziwi. Hili linajitokeza kwenye dondoo hii ya pete na nyanya yake;

> *‘‘Maisha yangu yalichukua mkondo mwingine nilipojiunga na darasa la saba kwani wajomba zangu hawakuchelea kupokea posa na mahari kutoka kwa buda mmoja aliyenioa kama mke wa nne. Maneno ya nasaha ya bibi yangu kuwajuza kuwa nilikuwa na hamu ya kufuatilia elimu na ni vyema niachwe nizime kiu yangu na kutimiza maazimio yangu yaliangukia masikio ya fisi.’’ (CLH-uk 148)*

Utafiti uliofanywa ulitambua kuwa kuna baadhi ya wanafanzi ambao baada ya kupata dhuluma kutoka kwa wazazi au walezi wao, huona maisha ya shuleni kuwa ombwe tupu kwao na hivyo kufanya maamuzi ya kukatiza elimu yao na kwenda zao. Vile vile, kuna wale wanaodhulumiwa na tamaduni za jamii zao na hivyo kufanya maamuzi mazito ya kukatiza elimu yao.

**Maisha Duni Shuleni**

Neno duni lina maana ya kiwango kidogo kilicho kinyume na matarajio. Pia ina maana ya ‘kilichokosa ubora’ wake asilia. Maisha duni ni ile hali ya kukosa ubora wa matarajio ya mtu. Kila mtu maishani huwa na hamu ya kuishi mazingira bora ili moyo wake upate kuridhika na kuwa na amani. Uduni wa aina yoyote ile hukosesha raha na hivyo kufanya kiumbe kukatizwa tamaa na hali yake. Mazingira ya shuleni na vyuoni ni mahali ambapo mwanafunzi yeyote yule huhitaji utulivu na ambapo utulivu ule unapokosekana kuna uwezekano mkubwa wa mwanafunzi yule kukatizwa tamaa na elimu na kufanya maamuzi ya kukatiza masomo yake. Mnamo Januari 2017, Shirika la Umoja wa Kimataifa linaloshughulika na elimu UNESCO liliripoti kuwa wanafunzi zaidi ya bilioni moja duniani wanakabiliwa na hali ngumu ya mazingira hasi shuleni hali inayowafanya baadhi yao kutamaushwa na hali hii na kutoroka shule. Shirika hili lilidai kuwa wanafunzi wengi na haswa wanaotoka kwa familia masikini au makabila, lugha na utamaduni wa walio wachache, wanaonewa na mitandao kote duniani na hivyo kuwa na wakaati mgumu wanapoendeleza masomo yao shuleni. UNESCO ilishauri kuwa ili watoto wawe na mazingira bora ya kusoma ni lazima washikadau wanaotangamana na masuala ya elimu wahakikishe kuwa ukatili na uonevu shuleni umenyimwa nafasi na kukomeshwa. Hili litajenga mazingira tulivu kwa wanafunzi kuandama elimu ya shuleni la sivyo wengi wao watazidi kukatiza masomo yao. Kauli ya shirika la

UNESCO haina tofauti na hali iliyobainika katika utafiti huu uliofanywa kutoka kwa riwaya teule za fasihi.

Assumpta Matei katika riwaya yake ya Chozi la Heri, anawaangazia wanafunzi wa chuo kikuu ambao wamekatishwa tamaa na mazingira duni chuoni hali ambayo inawafanya wakatize masomo yao na kujiingiza katika ulevi. Wanafunzi hawa wanadai kuwa kuna hali duni vyuoni kwani gharama ya masomo imekuwa ghali nayo halmashauri ya elimu inayojukumiwa kutoa mikopo ya masomo imeshindwa kutosheleza idadi kubwa ya wanafunzi walio na haja ya mikopo na ruzuku. Kutia msumari moto kwenye kidonda kibichi ni kuwa mikopo na ruzuku hizi hufaidi watoto wa matajiri huku wale wa maskini wakilazimika kufanya vibarua wakati wa likizo ili kujilipia karo na kugharamia mahitaji mengine ya kimsingi. Ukweli wa kauli hii unadhihirika kwenye dondoo ifuatayo ya mjadala wa wauguzi Selume na Meko pale hospitalini wakipishana zamu ya kuwahudumia wagonjwa;

> *''Nashangaa kinachompa kijana kama huyu na wengine waliofariki jana, ambao wanasomea shahada za uzamili, kujihusisha na unywaji wa pombe haramu…nasikia wanalewa ili kujipurukisha na hali duni ya maisha vyuoni.'' (CLH-uk 142)*

Utafiti huu ulibaini wazi kuwa kuna baadhi ya wanafunzi ambao hubidi kukatiza elimu yao ya shuleni pale ambapo mazingira ya shuleni huwa duni. Wanafunzi hawa hufa moyo na kutafuta mbinu zingine hasi za kutafuta utulivu wa maisha kwingineko na haswa kwenye nyanja za ulevi na dawa za kulevya.

**Kuiona elimu ya shuleni kuwa ngumu kwa kuilinganisha na anasa.**

Anasa ni hali au mambo ya starehe na raha nyingi iliyopita mipaka. Akili ya mwanadamu daima humdanganya kuwa anasa ni kitulizo salama cha moyo uliovurugika kwani huifanya akili kusahau mawi unayopitia na kuingia kwenye ulimwengu usio na taabu. Pindi binadamu anapokumbana na ulimwengu wenye uzito na uchovu wa maisha, hutafuta mazingira yatakomfanya kusahau dhiki anayopitia na kusaka raha kwingine ili aupe mwili wake utulivu wa muda. Kwa kiasi kikubwa mazingira ya elimu huwa magumu na hivyo pindi mwanafunzi anapokumbana na hali inayoweza kuutuliza moyo na mwili wake hutamaushwa na elimu na kujikuta kwenye hali ya kufuata raha. Katika karne ya ishirini na moja, kumetokea hali ambazo baadhi ya wanafunzi wameonekana kutamaushwa na elimu ya shuleni na kujiingiza kwenye maisha ya raha. Tuhuma za mapenzi miongoni mwa wanafunzi wakiwa shule sio jambo geni katika jamii ya sasa. Mnamo Septemba 2021, Wizara ya Jinsia na Utawala wa Mikoa nchini Tanzania iliripoti kuwa kuna idadi kubwa ya wanafunzi wanaojiingiza kwa anasa za mapenzi badala ya kuandama elimu iliyowapeleka shuleni. Wengi wa wanafunzi hawa huishia kuwa wajawazito na ili kuhofia aibu ya kujulikana na wenzao au walimu wao, hukatiza masomo yao na kuzamia anasa za kila aina zikiwemo ulevi na dawa za kulevya. Wanafunzi waliohojiwa na katibu wa wizara hiyo Martha Chilima walidai kuwa sheria nyingi za shuleni huwaumiza mioyoni kwa kuwanyima muda wao wa kujivinjari. Hivyo basi, wao hupenda kuwa na uhuru wa kufanya maamuzi yao bila vizingiti kutoka kwa walimu wao. Hali hii ndiyo iliyobainika katika utafiti uliofanywa na mtafiti katika utafiti huu.

Ken Walibora katika riwaya yake ya Kidagaa Kimemwozea anamwangazia mhusika Lowela ambaye aliamua kuachia masomo yake kidato cha tatu ili atumbue maisha kwani kifo chaweza kutokea kabla ya kuafikia azima yake. Licha ya kuwa wazazi wake walikuwa na uwezo wa kumwelimisha, Lowela alijiamulia kuwa elimu ya shuleni ingemnyima anasa alizozihitaji na hivyo kukinaizwa nayo na kuacha masomo. Lowela alimtumia kijana

mchunga ng'ombe kama tarishi wake wa siri aliyetumwa kupeleka na kurudisha nyaraka kwa wapenzi wake wa pembeni. Madai haya yanadhihirika kwenye dondoo iliyo hapa;

> *''DJ aliaminika sana na binti wa mwajiri wake Lowela na hivyo kuwa tarishi wake wa siri. Lowela alikuwa ameachia shule akiwa kidato cha tatu ili atumbue maisha angali hai maana kufa kwaja.'' (KK-uk 11)*

Mmojawapo wa wapenzi wa pembeni aliokuwa nao ni Mtemi Nasaba Bora ambaye baadaye alimpachika mimba. Lowela aliificha mimba kwa kuifunga kwa kitambaa kwa muda na pale alipoona kuwa haiwezi kufichika zaidi alifichwa na Mtemi Nasaba Bora kwenye mojawapo ya mashamba yake. Kitoto kilipozaliwa kilitupwa kwa mlango wa kibanda cha Amani ila baadaye kiliaga dunia.Vivyo hivyo, Walibora anamwangazia Mashaka bintiye Mtemi Nasaba Bora ambaye kupenda anasa ya mapenzi kulimnyima nafasi ya kuendelea na elimu ya shuleni. Huku angali shuleni, Mashaka alijihusisha na rafiki yake wa kiume Ben Bella. Mapenzi kati ya Mashaka na Ben Bella yalinata kiasi kwamba baada ya urafiki wao kufikia kikomo kwa ghafla, Mashaka anakuwa na wehu na kukatiza elimu yake ya shuleni akiwa kidato cha pili. Ukweli wa madai haya unajitokeza kwenye barua ya 'talaka' iliyoandikiwa Mashaka na Ben jinsi ilivyo katika dondoo hii;

> *''Nakumbuka miaka mingi iliyopita tulipokutana katika ukumbi wa mashindano ya densi ukiwa bado shule ya msingi. Nilianza kukupenda tangia hapo kwa moyo wa dhati na tukaahidiana kufunga ndoa hata kama ingebidi kusubiri miaka elfu baadaye.'' (KK-uk 80)*

Naye Assumpta Matei anamwangazia mwanafunzi wa kike Zohali ambaye anasa za mapenzi zilimlemea akiwa kidato cha pili na kujitosa kwenye raha iliyomfanya kuwa mjamzito. Ujauzito wa Zohali ulimlazimu mwalimu mkuu kumshauri dada yake Tima amrejeshe shuleni na akijifungua atafutiwe shule nyingine. Ukweli wa Zohali kulemewa na anasa badala ya kuandama elimu unajitokeza katika dondoo ifuatayo;

> *''Mambo yangu yalienda mrama nikiwa kidato cha pili. Niliikumbatia hali ya mtafaruku wa kihisia iwapatao vijana katika umri huu kwa papara za ujana. Kushtukia nilijipata nimeambulia ujauzito'' (CLH-uk 98)*

Kauli hizi zinadhihirisha wazi kuwa wanafunzi wengi hulinganisha elimu ya shuleni na anasa na kuiona isiyokuwa na faida kwao. Inawatamausha na kufanya maamuzi ya kuambata anasa na raha ili kujiliwaza kutoka dhiki na ugumu wa sheria za shuleni.

**Kutelekezwa na Walimu Wao**

Neno 'kutelekeza' lina maana ya kutompa huduma ya malezi inayohitajika. Hivyo basi kutelekezwa kwa wanafunzi na walimu wao ina maana ya walimu kutowajibika katika majukumu yao ya kutunza na kuwapa wanafunzi haki yao ya elimu. Hata hivyo, utafiti uliofanywa na kitengo cha habari cha NationMedia Group mnamo Aprili 2024 ulibaini kuwa baadhi ya walimu wanadai kuwa wanatelekeza majukumu yao kutokana na hatari wanazopitia katika mazingira ya kazi haswa shuleni. Kisa na maana,kuna wanafunzi wanaotumia dawa za kulevya na hata wao huungana pamoja kumwadhibu mwalimu pale anapojaribu kurudi mmoja wao. Hali hii huwaacha walimu kwenye njia panda haswa ikikumbukwa kuwa sheria za watoto daima humlinda mwanafunzi. Hili limewapa walimu kuwa na msimamo mmoja wa 'funza,nenda nyumbani' ili kuepuka lawama za kuwa na bugudha na wanafunzi. Hata hivyo,kuna baadhi ya walimu ambao hutelekeza majukumu yao ili kupata muda wao wa kutafuta starehe zao ili kutuliza nafsi zao mbali na mazingira ya

shuleni. Wanakosa muda wa kuwapa wanafunzi wao ushauri nasaha unaoweza kuwa wa msaada kwao.Pindi wanafunzi wanapogundua kuwa wametelekezwa na walimu,mara nyingi hutamauka na kukata kauli ya kujipa shughuli zao zilizo kinyume na elimu. Wengi wao hukatiza elimu na kujiingiza kwenye mikondo ya maisha ya kila aina kadri inavyodhihirika katika utafiti huu.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *KidagaaKimemwozea*,anawaangazia wanafunzi wa shule ya upili ya Nasaba Bora ambao kwa kuachiliwa na kupuuzwa na walimu wao wanatamaushwa na elimu ya shuleni na baada yake kuvuka vizingiti vya shule vilivyowekwa na walimu wao. Mwalimu Majisifu ambaye anapaswa kuwa shuleni akiwafundisha wanafunzi wasichana,anabaki nyumbani au kwenda kwa mama N'itilie kunywa pombe haramu. Wanafunzi wanabaki peke yao na kupata nafasi ya kuandama wapenzi wao badala ya kusoma. Kauli hii inadhihirika kwa maneno ya mwandishi akimrejelea mwalimu Majisifu kwenye dondoo ifuatayo ;

> *''Mwalimu Majisifu alishika njia kuelekea kwa mama Nitilie kutafuta maliwazo ingawa kilikuwapo kipindi kimoja cha kufundisha alasiri hiyo. 'Potelea pote. Sasa warembo hawa maziwa lala niwafundishe waende wapi ? Wacha wawe huru kuandika barua za mapenzi na wapange namna watakavyokiuka vizingiti vya shule na kuwafikia wapenzi wao wa pembeni.''(KK-uk 98)*

Vile vile,Walibora anamwangazia mwalimu huyu anayeitwa Majisifu kwa kuwatelekeza wanafunzi wake na kustareheka nyumbani kwake. Haya yanadhihirika kwenye mazungumzo ya Mwalimu na Mashaka aliyemtembelea nyumbani kumkabidhi barua ya kutoa mhadhara katika Chuo Kikuu cha Mkokotoni nchini Wangwani. Haya yanadhihirika kwenye sehemu ifuatayo ;

> *''Habari za masomo Mashaka ?'' Nzuri,ila twakuona darasani kwa nadra. Hatujasoma lolote katika somo la kiswahili karibu muhula wote. Tunakuta wewe uje utukomboe kutoka katika matatizo yanayotukumba darasani.''(KK-uk 47)*

Kauli hii inadhihirisha wazi kuwa kwa kupuuzwa na kutelekezwa na walimu wao kwa muda mwingi,wanafunzi walionekana kukatishwa tamaa na elimu hii na kuangazia masuala ya utovu wa nidhamu ya kuandikia wapenzi wao barua za wapendanao.

Kwa upande mwingine,mwandishi Assumpta Matei katika riwaya yake ya *ChozilaHeri*,anamwangazia mwanafunzi Zohali ambaye alikatishwa tamaa ya kuendelea na elimu ya shuleni na maneno ya mwalimu mkuu ambaye alimfukuza shuleni baada ya kupata ujauzito. Maneno ya mwalimu mkuu yalimvunja moyo Zohali kiasi cha kukata tamaa ya kuishi kwao na kutoroka nyumbani kwao na hata 'kuwaua'wazazi wake wangali hai. Kauli ya maneno mazito ya mwalimu mkuu inajitokeza kwa maneno ya Zohali kwa wenzake katika dondoo hii ;

> *''Maisha yangu yalianza kwenda mrama nilipojiunga na kidato cha pili kwani nilikumbatia maisha ya ujana kwa papara na kuambulia ujauzito. Sauti ya mwalimu mkuu ilitoa hukumu ya kifo kwa kumwambia dadangu kuwa nirejeshwe nyumbani na baada ya kujifungua nitafutiwe shule nyingine.''(CLH-uk 98-99).*

Kauli ya mwalimu mkuu aliyepaswa kutoa ushauri nasaha kwa Zohali ilimsumbua akilini hadi hata baada ya kujifungua alidinda kurudi masomoni kwa miaka miwili hadi pale alipotiwa moyo na Mtawa Pacha aliyemshauri kujiunga na shule ya upili ya Tangamano.

**Kuonewa Wivu na Wanafunzi Wenza**

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Jackline N. Murimi, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Maana ya kauli 'kuonewa wivu'ni hali ya kusikia maumivu na kutopendezwa na hatua zinazopigwa na wengine bila sababu yoyote ya kufanya hivyo. Wivu ina maana ya kuonea mtu kijicho au pia na kinyongo kwa sababu ya vitu vyao,utajiri wao wa mali au faida fulani wanayopata na ambayo imepiku ya wengine. Wivu huweza kutokea kwenye mazingira tofauti yakiwemo ya nyumbani,shuleni,maabadini,kazini na pia kwenye ulingo wa uongozi.

Mazingira ya shuleni huwa na wanafunzi wa aina tofauti na ambao wengine huwa na mitazamo potovu kuhusiana na maisha. Ingawa jamii huhitaji wanafunzi kutangama kwa muwala wa kujenga maisha yenye maono,sivyo ilivyo kwenye mazingira ya shuleni. Kuna baadhi ya wanafunzi ambao huonea wengine wivu labda kwa ufanisi wao masomoni ambapo mara nyingi huwa ni tabia ya kujifunza tu. Wanafunzi huoneana wivu kutokana na ufinyu wa akili unaotokana na masuala ya mapenzi,dawa za kulevya na hata ufanisi wa elimu.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *KidagaaKimemwozea* anamwangazia Amani ambaye alionewa wivu na wanafunzi wenza katika chuo kikuu.Wanafunzi husika walificha karatasi za uchochezi ndani ya chumba cha malazi cha Amani na kisha wakamwitia askari waliomkamata. Amani alitiwa jela kwa miaka mitano bila hatia,kifungo kilichomkosesha mazishi ya mama yake mzazi aliyefariki dunia kutokana na ajali ya barabarani. Hata baada ya kukamilisha kifungo chake,Amani alitamauka moyoni kabisa kiasi cha kuamua kutorudi chuoni na badala yake kufunga safari kuelekea Sokomoko kutafuta aliyemla jasho lake na aliyeiba mali ya familia yao. Kauli ya Amani kuonewa wivu na wanafunzi wenza inapatikana katika maneno yake mwenyewe kwa Madhubuti walipokuwa katika mjadala kuhusu usuli wao na falsafa zao kuhusu ukombozi katika dondoo ifuatayo ;

> *''Kusema kweli ni kuwa niliwahi kuwa chuo kikuu mjini Songoa. Kunao wenzangu walionionea gere kwa ufanifu wangu masomoni kwa kuficha karatasi za uchochezi chumbani mwangu na kisha kuniitia askari walionikamata na kufungwa jela kwa kipindi cha miaka mitano.'' (KK-Uk 117)*

Kwa upande mwingine,Assumpta Matei katika riwaya yake ya *ChozilaHeri*anamwangazia mhusika Ridhaa ambaye alionewa wivu na wanafunzi wenza wakiwa katika shule ya msingi kwani aliwashinda katika mitihani na kuwa mwanafunzi bora darasani mwao. Wanafunzi hawa walimchukia Ridhaa kiasi cha kumtenga na kumnyima nafasi ya kucheza nao katika mchezo wao wa 'kavuta' uliohusisha kusukuma vifuniko vya chupa za soda kwa ncha za vidole vya miguu. Walimsingizia wizi wa kalamu zao huku wakimpachika majina ya lakabu kama 'mfuata mvua'. Hali hii ilimvunja moyo Ridhaa na kukatishwa tamaa na masomo ya shuleni kiasi cha kumwambia mama yake kuwa hatorudi shuleni humo ima fa ima. Ukweli wa madai haya upo kwenye kauli ifuatayo ;

> *''Wewe ni mfuata mvua,hatutaki kucheza nawe. Umekuja kutushinda katika mitihani yetu,wewe ndiwe unayetuibia kalamu zetu. Ridhaa alichukua mkoba wake,akafulululiza moja kwa hadi nyumbani na huku akilia kwa shake akamwambia mama yake kuwa hangerudi shuleni tena.''(CLH-uk10).*

Ilimlazimu mama yake ridhaa kwenda shuleni siku iliyofuata ili kuzungumza na mwalimu kuhusiana na hali hiyo.

Kauli hizi zinadhihirisha wazi kuwa kuna baadhi ya wanafunzi ambao huchoshwa na kutamaushwa na elimu ya shuleni pale wanapoonewa wivu za wenzao kutokana na ufanisi wao katika masomo. Hali hii huwafanya kuchoshwa na elimu na kuambaa masomo hadi pale hamu yake inapojengwa na wao wenyewe au walezi wao ila baada ya muda fulani.

**Njia za Kukabiliana na Hali ya Wanafunzi Kutamaushwa na Elimu ya shuleni**

Waandishi wa riwaya za *KidagaaKimemwozea* na *ChozilaHeri* ambao ni Ken Walibora na Assumpta Matei mtawalia wanapendekeza baadhi ya mbinu mbalimbali za kupambana na hali nzito ya wanafunzi kutamaushwa na elimu shuleni. Hii ni kwa sababu wanafunzi wanapotamauka na kuwa watoro wa shule na vyuo,jamii huathirika moja kwa moja na kuwa athari zake zinaweza kuathiri hata vizazi vya baadaye kuhusiana na elimu. Baadhi ya mbinu za kukabiliana na hali ni zimejadiliwa hapa.

Kwanza,Ken Walibora anapendekeza kuwa baada ya vizingiti vilivyowafanya wanafunzi watamaushwe na elimu shuleni kufikia kikomo chake ni vyema mwanafunzi kurudi shule ili akamilishe masomo yake alipoyaachia. Ken anamwangazia mhusika Amani ambaye alikuwa amekatizwa tamaa na elimu baada ya wanafunzi wenza chuoni kuficha karatasi za uchochezi katika chumba chake na kumwitia askari. Baada ya safari ndefu yenye uchungu na kilio cha kusaka na kufanikiwa kuwapata walioiba mali ya familia yake pamoja na aliyemla jasho lake,Amani anaamua kurudi chuoni ili kukamilisha elimu yake alikoachia. Anarejea chuoni na baada ya miaka miwili alikuwa amejipatia shahada yake ya kwanza katika Fasihi na Falsafa(uk161).

Walibora pia anapendekeza kuwa ni vyema zaidi wanafunzi kutia bidii masomoni bila kujali hali zao duni walikotoka kwani usuli wa mja hauna uhusiano na mafanikio ya mwanafunzi elimuni. Anamwangazia mwanafunzi wa kiume Amani ambaye licha ya kutoka kwenye familia iliyokuwa na ufukara uliopita mipaka, alijikakamua masomoni hadi akaibuka miongoni mwa wanafunzi bora katika taifa la Tomoko kwa jasho lake mwenyewe akilinganishwa na mwenzake Fao aliyetoka kwenye familia tajiri na ambaye alifanyiwa mtihani(uk 36).

Pili,mwandishi Assumpta Matei anapendekeza kuwa wanafunzi walioathirika na utamaushi wa elimu ya shule wanapaswa kupewa ushauri nasaha ili wajenge moyo wa kuendelea na masomo yao. Matei anamwangazia msichana Mwanaheri ambaye baada ya kufiwa na mama yake na kukatizwa tamaa na elimu ya shuleni,mawazo yake huwa mazito kiasi cha kutangatanga anaposoma shuleni. Baada ya mwalimu wake Dhahabu kutambua kuwa Mwanaheri anakatizwa tamaa na elimu ya shuleni,anampa ushauri nasaha kuandama masomo yake kwani ndiyo nyenzo ya kumwezesha kuleta mabadiliko katika jamii(uk97).

Vile vile,Assumpta Matei anapendekezea jamii kushughulikia wanafunzi waliotamaushwa na elimu ya shuleni kutokana na ukosefu wa karo kwa kuwatafutia ufadhili kutoka kwa watu binafsi na mashirika yanayofadhili elimu ya watoto. Matei anamwangazia Zohali ambaye alitamausha na elimu ya shuleni akiwa kidato cha pili baada ya kupata ujauzito. Alipofukuzwa shuleni na mwalimu mkuu,Zohali alifanyishwa kazi nzito na wazazi wake na kukata kauli ya kutoroka nyumbani. Dhuluma kutoka kwa wazazi wake zilimuunguza mno kiasi cha 'kuwaua' wakiwa hai na kudai kuwa yeye ni yatima. Alikuwa amekula yamini kuwa hatorudi shuleni hadi pale alipopata ufadhili wa masomo kutoka kwa kituo cha Wakfu wa Mama Paulina chini ya uongozi wa Mtawa Pacha ambaye alimtafutia nafasi ya kuendelea na masomo yake katika Shule ya Upili ya Tangamano(uk100). Vile vile,Matei anamwangazia Chandachema ambaye alifadhiliwa na Shirika la Kidini la Hakikisho la Haki na utulivu ili kuendelea na elimu yake baada ya kukamilisha darasa la nane(uk 108).

Matei anazidi kupendekeza kuwa walimu wanaotelekeza wanafunzi wao na wengine kujiingiza katika anasa za mapenzi na wanafunzi hawa wanapaswa kupigwa kalamu. Kisa na maana ni kuwa walimu hawa huchangia wanafunzi husika kukatizwa tamaa na masomo pale

wanapopachikwa mimba na walimu wao. Anamwangazia Fumba aliyekuwa mwalimu wa Rehema na ambaye alipaswa kuachishwa kazi kama inavyofanywa nyakati hizi na badala yake alipewa uhamisho tu na kupelekwa shule nyingine.Adhabuya kuachishwa kazi kwa walimu hawa litakuwa funzo kwa walimu wengine wataokuwa na lengo la kuchangia ukataji tamaa wa elimu ya shuleni kwa wanafunzi(uk 103).

Vile vile,Matei anapendekeza kuwa ni vyema wanafunzi kujieleza kwa walimu wao pindi wanapofikia kiwango cha kukatizwa tamaa na elimu. Anamwangazia Chandachema ambaye walezi wake,anapiga moyo konde na kujipeleka kwa mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Kilimo. Huko alijieleza na kukubaliwa kuanza masomo yake katika darasa la pili(uk 105).

Hatimaye, Assumpta Matei anapendekeza kuwa ni vyema zaidi kwa wanafunzi wanaofikia kiwango cha kukatizwa tamaa na elimu ya shuleni kujikakamua wao wenyewe na kujitafutia hela za kujilipia karo haswa wakati wa likizo. Hii ni kwa sababu ongezeko la tamaa na ufisadi miongoni mwa viongozi kutoka kwa serikali, mara nyingi hufanya maamuzi duni na badala ya kutoa ruzuku kwa wanafunzi wanaotoka familia masikini, wao hushughulikia watoto kutoka familia zinazojiweza kiuchumi. Hili la wanafunzi masikini kutafuta karo wakati wa likizo linajitokeza katika maneno ya muuguzi Meko kwa mwenzake Selume(uk 142).

Mapendekezo yaliyojadiliwa hapo juu yanadhihirisha peupe kuwa endapo jamii itajifunga kibwebwe kukabiliana na matatizo yanayokumbana na wanafunzi kiasi cha kuwalazimu kuambaa elimu ya shuleni basi jamii ya kesho itakuwa na matumaini makubwa ya elimu.

## Hitimisho

Kutokana na utafiti uliofanywa imebainika kuwa kuna ongezeko la idadi ya wanafunzi waliotamaushwa na elimu ya shuleni kutokana na viini mbalimbali vinavyotokana na hali tofauti za maisha. Makala hii imeangazia kwa undani sababu zinazofanya wanafunzi watamaushwe na elimu shuleni na njia mwafaka za kukabiliana na hali hii kutoka kwenye vitabu teule na kwa jumla jamii pana kwani fasihi ni kioo cha jamii.

## MAREJELEO

Barasa,R.(2018). 'Mielekeo Ya Wanafunzi Na Wadau Wengine Wa Shule Za Sekondari Kuhusu Sheng' : Kifani Cha Shule Ya Upili Ya Jamhuri, Nairobi,Tasnifu Ya Uzamili', Chuo Kikuu Cha Nairobi

Kioko, A.N. & Muthwii, M.J. (2001).'*DemandsofaChangingSociety*: *EnglishinEducationinKenyaToday*. In Language, Culture and Curriculum 8(7):128.

Kisanji, J. (2013). Kufuwawa Kwa Miiko Na Kupotoka Kwa Maadili: "Uchunguzi Kifani Wa Jamii Ya Wabungu 'Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Kothari,R.(2004).*ResearchMethodology*: *MethodsandTechniques*.New Delhi:New age International (P) Limited Publishers.

Matei,A (2017)*ChozilaHeri*:Nairobi.One Planet Publishing & Media ServicesLimited.

Makoyo,M.S. (2014). ''*ACritiqueofChristianEducationforSelfRelianceinKenya*:*LightofExistentialism''*.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuucha Nairobi. (Haijachapishwa)Nairobi: OnePlanetPublishing&MediaServicesLimited

Mirianga, R (2014)''Mielekeo Ya Walimu Wa Shule Za Msingi Kuhusu Suala La Lugha Kama Linavyoelezwa Katika Katiba Ya Kenya'' Tasnifu Ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mohochi, S (2011) ''Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki Kuhusu Lugha ya Kiswahili''. Swahili Forum.

Mose,E. (2005) ''Taashira ya Kifo katika Tamthilia za '*MukwawawaUhehe'*, '*Amezidi'*, '*KiliochaHaki'* na '*Visiki''*.Tasnifu ya Uzamili.ChuoKikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa).

Mungah,C.(1999) "Dhana ya Maisha Katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi: *NagonanaMzingile*" Chuo Kikuu cha Nairobi. Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa).

Ogola,O. (1990) "Mielekeo ya Wanafunzi Kuhusu Elimu ya Shule za Upili Jijini Nairobi".Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta(Haijachapishwa).

Renatus, R (2017) ''Ujumi wa Kiafrika katika Tamthilia ya Kiswahili.Mifano kutoka *KinjekitilenaMashetani''*.Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa)

Republic of Kenya (1964) *KenyaEducationReportPart1* (Ominde Report). Nairobi: Government Printer.

Taylor, R (2021) *IntroductiontoCulturalAnthropology*. Boston, Allyn and Baccon, Inc
The Goverment of Kenya. (2010). *TheConstitution*. Nairobi: Goverment Publishers
UNICEF,UNHCR,(2013)''*KulindaWatoto* (*SavetheChildren*), na *MaonoDuniani* (*MaonoyaDunia*).*NjiaBorayaKuwalindaWatotoWote*: Nadharia na Mazoea ya Mfumo ya Kulinda Watoto, Ripoti ya Mkutano''.New Delhi, India: Mwandishi.

Walibora, K. (2012).*KidagaaKimemwozea*, Nairobi: Target Publication Limited
Wambui, H. (2017) "Uhusiano Wa Mbinu Za Ufundishaji Sarufi Na Umilisi,Mazungumzo ya Wanafunzi Wa Shule Za Msingi Za Umma Kaunti Ndogo Ya Kisumu Mashariki'' University of Nairobi.

Wamitila, K. W (2003) *KamusiyaFasihi* : *IstilahinaNadharia*. Nairobi : Focus Publication ltd.